**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI**

**Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 07 Juni, 2018.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ**:

52. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Mji wa Konde ni mji unaokuwa kwa kasi sana kama miji mengine ya Pemba. Hata hivyo, Mji huo hauna kituo cha kuegeshea magari maalum kwa sasa na hivyo, magari hupakia na kuteremesha abiria na mizigo kwenye njia panda ya Konde/Chake na Konde/Wete jambo ambalo ni hatari kubwa kwa usalama wa abiria.

(a) Je, Wizara ina mpango wa kukaa pamoja na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ili wakubaliane kujenga kituo cha magari (stand) ya abiria kwenye eneo la Wizara ya Kilimo lililokuwa likitumika kuogeshea ng'ombe.

(b) Je, ni lini Wizara italitatua tatizo la upatikanaji wa kituo cha magari (stand) Konde kama ilivyofanya katika miji ya Wete na Chake.

**Wizara ya Biashara na Viwanda:**

261. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Katika kuleta maendeleo kwa Zanzibar na wananchi wake Serikali imetilia mkazo suala la uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo. Hata hivyo, kukosekana kwa viwanda hivyo kunapelekea biashara ya vinywaji (juice) kutoka nje ya nchi kuingia kwa wingi hapa nchini na kupelekea kukosa kipato kwa Serikali na wakulima, kwani matunda hayo huharibika kwa muda mfupi bila ya kusarifiwa.

(a) Je, Serikali imejipangaje katika kulitatua suala la viwanda vya juice Zanzibar.

(b) Je, hatuoni kuna matunda hasa maembe yanapotea bure ikifika msimu wake na kukosa juice (*original*), mapato na ajira.

(c) Je, Serikali imejipanga na matunda gani ya kibiashara zaidi kuuza nchi za nje

**Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale:**

9. MHESHIMIWA SIMAI MOH'D SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kuwa Serikali inategemea kuendeleza uchumi wake katika kuendeleza Utalii na moja ya changamoto ya kuendeleza Utalii ni kuhakikisha ulinzi wa wageni pamoja na wawekezaji waliowekeza nchini.

(a) Ni kiasi gani cha fedha kinatumika kwa mwaka katika kuendeleza ulinzi huo huku ukizingatia polisi wanategemea fedha kutoka Jamhuri ya Muungano

(b) Kwa nini SMZ isianzishe Vituo vya Polisi kwa ajili ya wageni wanaotoka nchi za nje pamoja na mahakama za utalii ili kuweza kupata taarifa kwa haraka na waweze kukusanya ushahidi wa kutosha ili wageni hao wanapoondoka nchini pawe na uwezekano wa kuendesha kesi bila ucheleweshwaji

143. MHESHIMIWA SIMAI MOH'D SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kuwa mijadala inayoendeshwa ndani ya Bunge la Jamhuri inaigusa Zanzibar na wananchi kutoka Zanzibar wanakosa nafasi ya kuangalia moja kwa moja baada ya Serikali ya SMT kusitisha mijadala hiyo kuoneshwa MUBASHARA.

Je Wizara ya Habari, inachukua juhudi gani ili kuhakikisha Wazanzibari pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanapata fursa hiyo ya kuangalia mijadala ya Bunge Mubashara.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:**

156. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Pamoja na jitihada za Serikali kujenga barabara nzuri na kurahisisha usafiri wa nchi kavu, kumekuwa na changamoto ya alama za barabarani yakiwemo maeneo ya hatari katika barabara hizo na hivyo kusababisha ajali au madereva kuzozana na askari kwa kuwa alama hizo hazipo au hazitoshelezi.

(a) Kama hakuna alama za barabarani, Je, ipo Sheria ya Askari kumkamata dereva wa chombo.

(b) Je, kama alama hizo hazipo, hatuoni kuwa ndio ajali nyingi hutokea na kusababisha maafa.

(c) Je, kutokuweka miundo mbinu mizuri ya barabara na alama nani alaumiwe.

**Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:**

64. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) linastahili pongezi kwa kusambaza umeme kwa wananchi wa Unguja na Pemba. Pamoja na pongezi hizo, bado vipo vijiji vya Paje, Mwera na Jambiani ambako wananchi wameshafanya malipo lakini bado hawajaungiwa nishati hiyo.

(a) Kwanini maeneo hayo hayajaungwa umeme hadi leo.

(b) Hatua gani za haraka zitachukuliwa kuwafikishia huduma hiyo muhimu ya umeme.

**Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:**

129. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

Katika kuleta maendeleo ya michezo Zanzibar, ipo haja ya kuweka miundombinu bora zaidi ya michezo mbali mbali ili tuweze kuendeleza vipaji vya vijana wetu na kuwawezesha kupata ajira na kujipatia maendeleo na kuiletea sifa nchi yetu. Hata hivyo, bado tunaona ni mchezo wa mpira wa miguu pekee ndio uliopewa kipaumbele.

(a) Katika nchi yetu, ni mchezo gani unaoendana zaidi na utamaduni wetu.

(b) Mchezo wa ngumi hapa Zanzibar upo au haupo.

(c) Tuna mpango gani wa kuwatengeneza na kupeleka wachezaji wetu wa mpira wa miguu nje ya nchi.

**II. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka 2018/2019

**Zanzibar,**
**07 Juni, 2018.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**